

# Matokeo ya bipimo bya mazingira (environnement)

## Ju ya nini RDC?

Inchi ya **Kongo** iko na kazi mukubwa sana katika mabadiliko ya wakati ya ulimwengu. Mwaka wa 2024, RDC alitowa **76% ya kobalt na 13% ya shaba** ilitumikishwa ulimwenguni. Kipande kinene kya matokeo yale, kilitoka kwenye jimbo la **Lualaba**, dani ya **Kolwezi**, **Fungurume** na pembeni ya miji ile.

## Njia tulipitia ju ya iyi habari

**Mwenzi ya kumi 2025**, Source International RAID na Afrewatch balifanya bipimo bya pollution sababu ya kupata mahabari kwa ile inangariya pollution ile inatokeya kukuchimbula kwa kwivre na kobalt ku Lualaba. Tulipima pollution ya **hewa kwa mvumbi kigogo** ($PM_{2,5}$ na $PM_{10}$) tukapima **mvumbi inawaza kupumuliwa**, tena tukapima **mayi** na **matope** kutoka mitoni, bishima binatumikishwa na wakaji wa apa.

## Mayi na matope biko na pollution

### Mitoni na mabari



- **Kwivre** ilikuwa kichafuzi kikubwa kya mayi na matope.
- Biwango bya yulu bya **kobalt** na **manganeze** bilivumbuliwa
- Matope yalionesha alama wazi ya pollution ya maibwe. Katika mutoni wa **Musonoi**, kwivre ilkuwa na 34 mg/kg mbele ya mafaniko ya mungoti ilikuwa 2100 mg/kg.

***HATARI INANGARIYA ILE MAMBO:***
*sumu kwa biumbe bya mu mayi, biumbe binakufwa dani ya mayi.*

### Mahi ya mu nyumba



- Bishima bya mingi bilikuya na biwango.
- Bishima byote bilikuwa **mara 100 na aside kuliko vile OMS inaomba**.



- Kishima kilichimbuliwa 200 metre karibu na fasi ya buchafu bwa maibwe, kilikuwa na 1100 µg/L ya **manganeze** au mara 14 ya kipimo kiliwekwa na OMS.

***HATARI INANGARIYA ILE MAMBO:***
*mayi ya aside yanaweza kutosha byuma na kongenza magumu.*

## Byuma bwa buzito byenye washiwashi na atari ju ya afya

**Cu** — **Kwivre**
Inaleta magonjwa ya estoma; na ya mafwafwa

**Co** — **Kobalt**
Inaleta magonjwa ya estoma ; ya na roho

**Mn** — **Manganeze**
Inatosha maefe ya ku akili na inakosesha kukomala kuzuri kwa batoto







# Pollution ya hewa irikuya ya kawaida na fasi yoyote

**Bipimo byote bya kila siku biryanzakutambuka mitindo ya OMS bya $PM_{2,5}$ ata bya $PM_{10}$.** Bipimo bya $PM_{2,5}$ bya kila siku bilikuya kati ya 33 paka 87 µg/m$^3$ (lakini kipimo kinaombwa na OMS ni 15 µg/m$^3$), sababu kya $MP_{10}$ kilikuwa ni 67 ata 178 µg/m$^3$ (kipimo kinaombwa na OMS ni 45 µg/m$^3$). Matokeyo aya ayatokeye tu kwa kushituka: **maonesho ya saa inaonesha kama pollution ilikuwa yulu sana bushiku buzima** Na kilele zaidi muchana na mangaribi katika masite ya karibu na mingoti ya wazi. Na site inyekuchafusiwa sana, iko pa 500 metre na depo COMMUS ya ku Kolwezi, na ile site ilikuwa na hewa ya mubaya mbele ya bantu bonte.

**Bipimo bya $PM_{2,5}$ bya kila siku kwa eneo (µg/m$^3$)**




**98%** **Bipimo bya saa ya $PM_{2,5}$ bilipita maagizo ya OMS**

**84%** **Bipimo bya saa ya $PM_{10}$ bilipita maagizo ya OMS**

**7/8** **Masite iko na hewa mubaya bele ya bantu beko déjà mumagumu**




## Galaxy: Masomo yenye kuzungukwa na mingoti

Masomo ya Galaxy ku Kolwezi iko na banafunzi 1700 na yeko pembeni ya mingoti ya COMMUS

| | | |
|---|---|---|
| $PM_{2,5}$ | **3x** | ya maagzo ya OMS |
| $PM_{10}$ | **2x** | ya maagizo ya OMS |
| Kwivre na kobalt katika mvumbi | **4x** | ya maagizo ya elimu vile inasema mvumbi ikuwe bila atari |

## Je, tunajuwa kama ni pollution inatoka ku mingoti?

Tulipima maonyesho ya mvumbi inaweza kupumuliwa. Miungo yao ilikuya yakwachana na mvumbi ya kila siku dani ya miji: ilikuwa na kwivre, kobalt na manganeze zaidi ya kawaida. Ile inaonesha kama ile mvumbi itatoka pa madepo ya maibwe kama mpempo inalamuka. **Na akuna maagizo yenye wazi, sababu mvumbi ya kwivre na kobalt inapita mipaka ya ile inawekwa ju ya afya ya binadamu**.

**KWA KUJUWA SANA:** MUNAWEZA KUSKANE QR JU YA KUONA MARAPOR YOTE PA WWW.SOURCE-INTERNATIONAL.ORG

**GAWANYENI PEMBENI YENU MATOKEYO AYA !**

